LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar es Salaam, Tanzania
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## MAONI JUU YA RASiMU YA SERA YA ELIMU TOLEO LA MWAKA 2023

Dar Es Salaam, 11 Mei 2023

## 1.0 Utangulizi

Ndugu wanahabari,

Mtakumbuka kwamba mwaka 2014 serikali ya Tanzania ilizindua sera mpya ya elimu ikiifuta iliyokuwa sera ya elimu na mafunzo mwaka 1995, LHRC ikiwa mdau muhimu katika sekta ya elimu ilishiriki katika mchakato mzima wa upatikanaji wa sera hii kwa kuamini kwamba hakuna Taifa bora kama watu wake hawana elimu ya kutosha, kama ambavyo mwasisi wa Taifa hili Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wakati akizungumza na walimu mwaka 1969 alizungumzia dhana ya elimu, naomba kununukuu, *"„,Walimu mkiendelea kuwa watu wa kutayarisha watu wa kufanya mitihani mtakuwa watu wa kikoloni kabisa nyie, lazima muwe walimu wa kufundisha watu kuibadili Afrika, elimu ni lazima iwe na lengo na mtazamo wa kimapinduzi na kifikra na sio elimu ya kufaulu mitihani na kupata cheti"„,.*Mwisho wa kunukuu

Ndugu wanahabari,

Hata hivyo, baada ya sera hiyo kuzinduliwa, bado ilionekana kuwa na mapungufu kadha wa kadha, hii ilitokana na wadau wa elimu nchini kutofautiana kimawazo na kimtazamo juu ya sera hiyo.

Ndugu wanahabari,

Baada ya wadau kuwa na maoni tofauti tofauti juu ya sera hiyo huku wakitoa wito kwa serikali kuifanyia mapitio sera hiyo, hatimaye mwaka 2022, Serikali kupitia Waziri mwenye dhamana ya elimu Mhe Prof. Adolf Mkenda iliutangazia umma kuwa imeamua kufanya mapitio ya sera ya elimu toleo la mwaka 2014 pamoja na mitaala yake yote.

Ndugu wanahabari,

Baada ya uamuzi huo wa Serikali, LHRC iliamua kufanya mapitio na uchambuzi wa sera ya elimu ya mwaka 2014, baada ya uchambuzi huo, LHRC iliwasilisha kwa maandishi uchambuzi huo wizara ya elimu mwezi Mei mwaka 2021.

Ndugu wanahabari,

Baada ya LHRC kuwasilisha uchambuzi huo, wizara kupitia ofisi ya katibu mkuu ilitujibu kwa maandishi kuwa timu ya wataalamu kutoka wizarani hapo ilikuwa ikifanya kazi inayofanana na hio hivyo tungepata mwaliko wa Kwenda kuwasilisha mapendekezo yetu mbele ya menejimenti ya wizara pindi timu ya wataalumu kutoka wizarani itakapokamilisha kazi yake.

Ndugu wanahabari,

Baada ya timu ya wataalamu kutoka wizara ya elimu kukamilisha kazi yake, mnamo mwezi Oktoba mwaka 2022, LHRC ilipokea mwaliko kutoka wizara ya elimu Kwenda kuwasilisha mapendekezo ya mapitio ya sera ya elimu 2014 mbele ya menejimenti ya wizara iliyokuwa ikiongozwa na Waziri mwenye dhamana ya elimu Mhe Prof. Adolf Mkenda pamoja na aliyekuwa katibu mkuu wa wizara hiyo dr. Francis Michael, ambapo LHRC iliwasilisha mapendekezo yake kwa mujibu wa mwaliko.

Ndugu wanahabari,

Ni takribani miezi sita(6) sasa tangu LHRC iwasilishe mapendekezo yake wizarani ambapo tarehe 9 Mei Waziri wa elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe Prof. Adolf Mkenda alijitokeza mbele ya vyombo ya habari na kuujulisha umma wa watanzania kuwa mchakato wa mapitio ya sera ya elimu toleo la 2023 umekamilika na kwamba rasimu ya kwanza ya sera ya elimu imekamilika na wadau wanakaribishwa kutoa maoni juu ya rasimu hiyo, ambapo pamoja na mambo mengine kutafanyika kwa kongamono kubwa la wadau wa elimu kwa ajili ya kukusanya maoni litakalofanyika tarehe 11 hadi 14 mwezi Mei 2023 katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Conventional Centre jijini Dodoma.

## 2.0 Mapendekezo ambayo LHRC tunakubaliana na Rasimu ya sera

- Ukomo wa elimu ya msingi, sekondari na elimu ya juu

Ndugu wanahabari,

Kwa mujibu wa rasimu ya sera ya elimu toleo la mwaka 2023, inapendekeza kuwa na mfumo wa elimu wa 1+6+4+2/3+3+,, kwa maana ya kwamba elimu ya awali au chekecheka itakuwa kwa kipindi cha mwaka mmoja, elimu ya shule ya msingi itakuwa kwa kipindi cha miaka sita(6) tofauti na sasa ambapo elimu ya msingi ni ya kipindi cha miaka saba(7), elimu ya sekondari ya chini kwa maana ya kidato cha kwanza mpaka cha nne itabaki kuwa miaka minne, elimu ya sekondari ya juu kwa maana kidato cha tano na sita itabaki kuwa miaka miwili, na elimu ya chuo kikuu itakuwa kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu na kuendelea,

- Elimu ya msingi na elimu ya sekondari ya chini kuwa lazima

Ndugu wanahabari

Kwa mujibu wa rasimu ya sera ya elimu inapendekeza elimu ya msingi na elimu ya sekondari ya chini kwa maana ya kidato cha kwanza hadi cha nne itakuwa ya lazima ambapo itatolewa kwa miaka kumi(10) kwa maana ya miaka sita ya shule ya msingi na miaka minne ya kidato cha nne, haitokuwa hiari tena, tofauti na sera ya sasa ambapo elimu ya lazima ilikuwa ya msingi pekee.

- Elimu ya amali na elimu ya amali sanifu

Ndugu wanahabari

Kwa mujibu wa sera ya elimu ya sasa, mfumo wa elimu amali maarufu kama QT ambapo wanafunzi wenye alama ndogo zisizowaruhusu kujiunga kidato cha tano na sita husoma kwa miaka miwili vidato vyote vinne ambapo kwa jina jingine hujisajili kama watahiniwa binafsi( private candidates) haukuwa mfumo rasmi kwa mujibu wa sera ya elimu ya sasa, ambapo rasimu ya sera ya elimu inapendekeza kuuingiza mfumo huu, sasa kuwa mfumo rasmi wa elimu hapa nchini.

- Elimu ya amali sanifu

Ndugu wanahabari,

Elimu ya amali sanifu kwa maana ya wanafunzi waliokuwa wakimaliza kidato cha nne wakiwa na ufaulu wa chini ambao hauwaruhusu kujiunga na kidato cha tano walikuwa wakitakiwa kujiunga na mafunzo ya cheti cha astashahada(certificate) baadae mafunzo ya cheti cha stashahada( diploma) na ndipo wajiunge na elimu ya juu kwa maana ya chuo kikuu, mfumo huu haukuwa mfumo rasmi kwa mujibu wa sera ya elimu ya mwaka 2014.

Rasimu ya sera ya elimu tolea la mwaka 2023 inapendekeza kuutambua mfumo huu rasmi katika mifumo ya elimu hapa nchini ambapo elimu ya amali sanifu itakuwa hitaji la lazima ili kujiunga na elimu ya juu, kwa lugha nyingine mwanafunzi mwenye shahada iliyotokana na mkondo wa kidato cha sita na mwanafunzi mwenye shahada iliyotokana na mkondo wa elimu ya amali sanifu wote watakuwa na shahada zenye uzito sawa.

- Umri wa kuanza darasa la kwanza

Ndugu wanahabari,

Kwa mujibu wa sera ya elimu ya mwaka 2014 umri wa kuanza darasa la kwanza ulikuwa miaka kumi na moja, ambapo sasa rasimu ya elimu inapendekeza umri wa kuanza darasa la kwanza kuwa miaka sita(6),.

- Elimu bure

Ndugu wanahabari,

Kwa mujibu wa sera ya elimu ya mwaka 2014, elimu ya msingi hadi kidato cha nne kwa shule za umma ni bure kwa maana ya elimu bila malipo, hata hivyo serikali ya awamu ya sita(6) ilitangaza kufuta ada kwa ngazi ya sekondari kidato cha tano na sita kwa maana ya elimu bure, rasimu ya sera

ya elimu toleo la mwaka 2023 inapendekeza kuwa elimu bila malipo itakuwa kuanzia shule ya msingi hadi kidato cha sita.

- Matumizi ya taknolojia katika elimu na mafunzo

Ndugu wanahabari,

Kwa muda mrefu wadau wa elimu tumekuwa tukisisitiza matumizi ya teknolojia katika elimu ya Tanzania, hata hivyo suala hili halikuwa suala la kisera, rasimu ya sera toleo la mwaka 2023 inapendekeza matumizi ya TEHAMA katika ngazi zote za elimu,

- Lugha ya kufundishia

Ndugu wanahabari,

Kwa mujibu wa rasimu ya elimu toleo la mwaka 2023 inapendekeza kuwa Lugha ya Taifa Kiswahili itatumika kufundishia katika elimu ya awali na elimu ya msingi pekee isipokuwa masomo ya lugha za kigeni na katika shule zitakazoomba kutumia lugha ya kingereza kufundishia, Lugha ya Kingereza itatumika kufundishia kuanzia ngazi ya sekondari ya chini isipokuwa somo la Kiswahili.

- Mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu na Watoto wa kike

Ndugu wanahabari,

Moja ya changamoto kubwa tuliyokuwa nayo katika mifumo yetu ya kielimu ni changamoto za kielimu kwa wanafunzi wenye ulemavu na wasichana zikiwemo changamoto za kimahitaji, changamoto ambazo hata sera ya elimu toleo la mwaka 2014 haikuzitolea ufumbuzi changamoto hizi, kwa muda mrefu wanafunzi wenye ulemavu wamekuwa na changamoto ikiwemo mahitaji ya maandishi ya nukta nundu katika ngazi zote za elimu na mazingira rafiki ya kujifunzia kwa Watoto wa kike. Rasimu ya sera toleo la mwaka 2023 inapendekeza kuwepo kwa maandishi ya nukta nundu kwa wanafunzi wenye ulemavu katika ngazi zote za elimu sambamba na mazingira rafiki ya kujifunzia kwa Watoto wa kike.

3.0 Hitimisho

- Mambo ambayo Sera haijayazingatia

Ndugu wanahabari

Mwisho lakini sio kwa umuhimu napenda kutoa mapendekezo ambayo rasimu ya sera haijayazingaita kabisa kama ifuatavyo

i. Baadhi ya taasisi kama vile maafisa elimu utamaduni, maafsa elimu taaluma, maafsa elimu TEHAMA na maafsa elimu sekondari kutotambuliwa na rasimu ya sera licha ya nafasi hizo kuwepo katika mfumo wa elimu nchini, tunapendekeza nafasi hizo zitambuliwe na sera au kama hazipo kwenye muundo wa kiutawala zifutwe

ii. Rasimu ya sera itoe ufafanuzi wa kina juu ya dhana ya elimu isiyo katika mfumo rasimi ni elimu ya namna gani ili kuondoa mchanganyiko uliopo mpaka sasa
iii. Rasimu ya sera ieleze ni namna gani wanafunzi waliopitia katika mkondo wa elimu isiyo rasimi watatambuliwa kwenye mfumo wa elimu rasimi
iv. Rasimu ya sera ieleze endapo sera hii itatumika katika elimu ya juu ili kuondoa mchanganyiko uliopo katika sera ya elimu ya sasa kutokana na kutokuweka bayana kama inatumika katika ngazi ya elimu ya juu au haitumiki.
v. Rasimu ya sera ya elimu ifungamanishwe na sera nyinginezo zinazoongelea kwa namna moja ama nyingine ujuzi na maarifa kama vile sera ya sayansi na teknolojia, sera ya viwanda vidogovidogo ili kuwa na zao la wahitimu wenye ujuzi na maarifa zaidi.
vi. Muda wa kutosha wa kupitia, kuchambua, kuchakata na kufanya mapitio ya rasimu ya sera utolewe kwa wadau tofauti na sasa ambapo wizara imetoa muda wa wiki tatu pekee, muda ambao unaweza usitoshe, lengo ni kuhakikisha Taifa letu linapata sera iliyo bora na inayokidhi kiu na matarajio ya watanzania.
vii. Kuwe na kipegele cha kufanya tathimini kila baada ya miaka 10 juu ya utekelezaji wa sera.
viii. Dhana ya elimu bila malipo iwekwe bayana kutokana na ukweli kwamba lugha iliyotumika katika rasimu inaashiria dhana ya elimu bila malipo kutokuwa bure kiuhalisia, lugha iliyotumika inaashiria Dhahiri shahiri kuwa elimu haitokuwa bure bali kutakuwa na michango kadhaa.
ix. Rasimu itoe mwongozo wa adhabu ya viboko kutokana na ukweli kwamba haijagusia kabisa suala hili
x. Suala la Watoto wa kike kurudi mashuleni baada ya kupata ujauzito liwe la kisera kutokana na ukweli kwamba rasimu ya sera haijalizungumzia kabisa suala hili.

Imetolewa na:

Dr. Anna Henga(Wakili)

Mkurugenzi Mtendaji.

Board of Directors:
Hon. Chief Justice (Ret'd) Barnabas A. Samatta - Chairperson, Ms. Anastazia Rugaba - Vice Chairperson,
Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Rebeca Z. Gyumi - Member,
Ms. Sophia M. Komba - Member, Dr. Abdullah H. Mohammed - Member, Ms. Josephine A. Zimba - Member,
Ms. Lutgard Kokulinda Kagaruki – Member, Dr. Ally Hussein Laay - Member